**MUHUTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 25.10.2021**

MAHUDHURIO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Neema Kapesa | M/kiti |
| 2. | Emmanuel Sulo | katibu |
| 3. | Joel Mkuchika | mjumbe |
| 4. | William Mpangala | mjumbe |
| 5. | Tumaini Mgaya | mjumbe |
| 6. | Malyago Leticia | Mwanasheria |

SECRETARIETI

1. Leodigadius Katabalo
2. Mtaka Membe
3. John Mabara

AGENDA ZA KIKAO

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda za kikao
3. Kupitia muhutasari wa kikao cha 10/08/2021
4. Kuridhia Ujenzi wa kituo cha AfyaTumbi kwa njia ya force account ( Maabara, Upasuajina Mama na Mtoto) kiasi kilichotengwa ni Tsh. 300,000,000.00
5. Kuridhia ujenzi wa madarasa kwa njia ya force account katika shule za msingi Inala, Kanyenye, Masimba na Kiyungi) kiasi Kilichotengwa ni Tshs. 112,500,000.00
6. Kuria Ujenzi wa madarasa 74 Shule za sekondari na Msingi Manispaa ya Tabora kwa njia ya force account kiasi kilichotengwa Tshs. 1,480,000,000.00
7. Kuridhia ombi la kutangaza zabuni ya mgahawa wa Manispaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022
8. Kufunga kikao

KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 10.00 alasiri baada ya akidi lazimu ya wajumbe kutimia.

**MUH. NO 3/2021/2022/2 UJENZI WA KITUO CHA AFYATUMBI ( MAABARA, UPASUAJINA MAMA NAMTOTO) KIASI KILICHOTENGWA NI TSH. 300,000,000.00**

Bodi ya Zabuni imepitia BOQ pamoja na mapendekezo ya Kitengo cha Ununuzi juu ujenzi wa jengo la Maabara,Upasuaji na OPD katika Kituo cha Afya Tumbi na kuridhia ununuzi huu ufanyike kwa kuzingatia bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pia Ujenzi huu ufanyike kwa utaraibu wa *Force Account*na mradi huu utekelezwe ngazi za chini *(Lower Level)*

**MUH. NO 3/2021/2022/3 UJENZI WA MADARASA SHULE YA MSINGI ( INALA, KANYENYE, MASIMBA NA KIYUNGI) KIASI KILICHOTENGWA NI TSHS. 112,500,000.00**

Bodi ya zabuni ilipitia kwa kina mapendekezo ya Kitengo cha Ununuzi na Ugavi na kuamua kuwa ununuzi huu wa majenzi ufanyike kwa utaratibu wa *Force Account* pia miradi hii itekelezwe ngazi za chini hata hivyo, wajumbe wa bodi wameridhia kazi hizi zifanyike kwa mgawanyo ufuatao:-

i. Umaliziaji wa vyumba vinne (4) vya madarasa Shule ya Msingi Inala kiasi kilichotengwa Tshs. 50,000,000.00

ii. Umaliziaji wa chumba Kimoja (1) cha darasa Shule ya Msingi Kanyenye kiasi kilichotengwa 12,500,000.00

iii. Shule ya Msingi Masimba kiasi kilichotengwa ni Tsh. 12,500,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wachumba cha darasa moja (1)

iv. Shule ya Msingi Kiyungi kiasi kilichotengwa 37,500,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa nyumba vya madarasa vitatu (3)

Aidha, wajumbe wamesisitiza kuwa fedha hizo zikamilishe umaliziaji wa madarasa hayo pamoja na ununuzi wa madawati.

**MUH. NO 3/2021/2022/4 UJENZI WA MADARASA 74 SHULE ZA SEKONDARI NA MSINGI MANISPAA YA TABORA KIASI KILICHOTENGWA TSHS. 1,480,000,000.00**

Bodi ya zabuni ilipitia mapendekezo ya Kitengo cha Ununuzi na Ugavi na kuamua kuwa ununuzi huu wa majenzi ufanyike kwa utaratibu wa *Force Account* pia miradi hii itekelezwe ngazi za chini, hata hivyo, wajumbe wa bodi wameridhia ununuzi huu kwa mgawanyo ufuatao

1. **SHULE ZA SEKONDARIUJENZI WA MADARASA 60**

i. Shule ya Sekondari Nkumba ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

ii. Shule ya Sekondari Chang'a ujenzi wa vyumba vya madarasa vitatu(3) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 60,000,000.00

iii. Shule ya Sekondari Kaze Hill ujenzi wa vyumba vya madarasa vitano(5) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 100,000,000.00

iv. Shule ya Sekondari Ndevelwa ujenzi wa vyumba vya madarasa vitatu(3) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 60,000,000.00

v. Shule ya Sekondari Sikanda ujenzi wa vyumba vya madarasa vitatu(3) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 60,000,000.00

vi. Shule ya Sekondari Bombamzinga ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa (4) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 80,000,000.00

vii. Shule ya Sekondari Nyamwezi ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

viii. Shule ya Sekondari Kanyenye ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

ix. Shule ya Sekondari Kariakoo ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

x. Shule ya Sekondari Fundikira ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa (4) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 80,000,000.00

xi. Shule ya Sekondari Kalunde ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa (4) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 80,000,000.00

xii. Shule ya Sekondari Itonjanda ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

xiii. Shule ya Sekondari Itetemiaujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

xiv. Shule ya Sekondari Isevya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa (4) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 80,000,000.00

xv. Shule ya Sekondari Ipuli ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa (5) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 80,000,000.00

xvi. Shule ya Sekondari Ikomwa ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

xvii. Shule ya Sekondari Lwanzali ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

xviii. Shule ya Sekondari Kazima ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

xix. Shule ya Sekondari Cheyo ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

**2. SHULE ZA MSINGI SHIKIZI UJENZI WA MADARASA 14**

i. Shule Shikizi Usule ujenzi wa vyumba vya madarasa sita (6) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 120,000,000.00

ii. Shule Shikizi Tumbi ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

iii. Shule Shikizi Farm Nyamwezi ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

iv. Shule Shikizi Kilino ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

v. Shule Shikizi Timkeni ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili (2) Kiasi kilichotengwa ni Tshs. 40,000,000.00

Aidha, wajumbe wa Bodi ya Zabuni wamesisitiza kuwa fedha hizo zikamilishe ujenzi wa madarasa hayo pamoja na ununuzi wa madawati

**MUH. NO 3/2021/2022/5 OMBI LA KUTANGAZA ZABUNI YA MGAHAWA WA MANISPAA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

Bodi ya zabuni imepitia mapendekezo ya Kitengo cha Ununuzi na Ugavi na kuamua kuwa zabuni hii itangazwe haraka .

**MUH. NO 3/2021/2022/6 KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti alifunga kikao saa 11.30 jioni baada ya agenda zote kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

## UMETHIBITISHWA

MWENYEKITI
.........................
SAHIHI
....11/04/2022........
TAREHE

KATIBU
.........................
SAHIHI
....11/04/2022........
TAREHE